



## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

### TOZO MPYA ZA HIFADHI ZA TAIFA KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

**Arusha, Julai 30, 2020**

Shirika la Hifadhi za Taifa linapenda kutangaza mabadiliko ya tozo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambayo yanahusu maeneo makuu matatu (3) kama yalivyobainishwa hapa chini. Tozo hizi zitaanza kutumika rasmi kuanzia Agosti Mosi, 2020 hadi Juni 30, 2021 na pia hakuna mabadiliko kwa tozo zilizokuwa zikitumika hapo awali.

#### **(i) Multiple entry fee**

Tozo hii sasa itaanza kutumika mwaka huu wa fedha. Tozo hii itakuwa ya namna mbili, kibali (permit) cha saa 12 kwa wageni wanaolala nje ya hifadhi na kibali (permit) ya saa 24 kwa wale wanaolala ndani ya hifadhi. Katika tozo hizo mbili viwango stahiki vya tozo kwa kila hifadhi vitatumika.

Aidha, tofauti iliyopo kati ya vibali hivyo viwili ni kuwa kibali cha saa 12 kitaisha (expire) inapofika saa 12 jioni bila kujali ilikatwa muda gani wa siku husika. Ndani ya muda wa "permit" ya saa 12 mgeni anaweza kutoka na kurudi hifadhini bila kulipia tozo ya ziada. Kwa upande mwingine kibali cha saa 24 kitadumu kwa kipindi cha saa 24 tangu kilipotolewa na ndani ya muda huo, mgeni anaweza kutoka na kurudi hifadhini bila kulipa tozo ya ziada.

Uamuzi huu wa Serikali unalenga kuinua utalii wa kiutamaduni kwenye maeneo ya wananchi yaliyoko nje ya Hifadhi za Taifa ambapo wageni hasa watalii walishindwa kuyatembelea kwa kuhofia kulipia tozo mara mbili. Uamuzi huu sasa unatarajiwa kuinua utalii wa kiutamaduni kwenye maeneo hayo pamoja na kuongeza kipato cha wananchi katika maeneo hayo na hivyo kufaidika na uwezo wa hifadhi katika maeneo wanayoishi.

**(ii) Punguzo la Tozo kwa Baadhi ya Bidhaa za Utalii**

Katika jitihada za kuvutia watalii kutembelea hifadhi, Serikali imepunguza tozo kwa baadhi ya bidha za utalii kama vile Canopy walk way Ziwa Manyara kufikia kiasi cha US\$ 20 kutoka US\$ 60 kwa wageni wa nje na TZS 10,000/- kutoka TZS 15,000/- kwa wakazi wa Afrika Mashariki.

**(iii) Tozo kwa Hifadhi Mpya**

Kufuatia uamuzi wa serikali wa kuanzisha hifadhi mpya za Burigi-Chato; Ibanda - Kyerwa na Rumanyika-Karagwe; Ugalla River, Nyerere na Kigosi mwaka 2019. Tozo kwa hifadhi hizi nazo ni miongoni mwa zilizotangazwa katika taarifa hii.

Mabadiliko haya ya Tozo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 yametokana na Matangazo ya Serikali Namba: 666 (2018); 490A (2020) na 181 (2016) ambayo yote kwa pamoja yanalenga kuongeza idadi ya watalii, mapato pamoja na kuboresha huduma za utalii ndani ya hifadhi.

Jedwali lenye tozo kwa mwaka huu wa fedha limeambatishwa kwenye taarifa hii.

Imetolewa na:



Pascal Shelutete

**Kamishna Msaidizi Mwandamizi – Mawasiliano**